



WIZARA YA ELIMU , SAYANSI NA TEKNOLOJIA

TANGAZO

UFADHILI WA MASOMO YA SHAHADA YA UZAMILI KWENYE FANI ZA SAYANSI YA TAKWIMU NA AKILI UNDE (DATA SCIENCE AND ARTIFICIAL INTELIGENCE) KATIKA TAASISI YA TEKNOLOJIA YA INDIA MADRAS, KAMPASI YA ZANZIBAR KUPITIA PROGRAMU YA SAMIA (SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED DS/AI+) MWAKA WA FEDHA 2026/2027

A. UTANGULIZI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza program maalum ya **SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED DS/AI+** inayolenga kuongeza na kukuza ujuzi wa vijana wa Kitanzania katika fani za Sayansi ya Takwimu, Akili Unde na Sayansi Shirikishi (Data Science, Artificial Intelligence and Allied Sciences) kulingana na mahitaji ya soko la ajira nchini na kuchangia katika maendeleo ya Taifa, Kikanda na Kimataifa.

Wizara inatangaza fursa za ufadhili wa masomo katika ngazi ya **Shahada ya Uzamili** kwa wahitimu wenye ufaulu wa juu zaidi kwenye masomo ya *Data Science, Artificial Intelligence, and related disciplines* kama vile *Machine Learning, Cybersecurity, Computer Science, Computer Engineering, and Software Engineering*.

B. MAENEO YA UFADHILI

SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED DS/AI+ itatoa ufadhili kwa ajili ya masomo ya shahada ya uzamili unaojumuishia:

- Ada ya Mafunzo kwa
- Posho ya chakula na malazi
- Posho ya Vitabu na Viandikwa
- Mahitaji Maalum ya Vitivo
- Utafiti
- Bima ya Afya

C. VYUO VIKUU VINAVYOLENGWA

Ufadhili utatolewa kwa waombaji wenye udahili katika **Taasisi ya Teknolojia ya India** ya (Indian institute of Technology Madrasa (IITM)) Kampasi ya Zanzibar.

D. MUDA WA UFADHILI

Wanafunzi watakaofadhiliwa, watagharimiwa kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha 2026/27.

E. SIFA ZA WAOMBAJI WA UFADHILI

Ufadhili huu utatolewa kwa wanafunzi waliohitimu shahada ya kwanza wenye sifa zifuatazo:

- i) Awe Mtanzania.
- ii) Awe na udahili wa kusoma Shahada ya Uzamili katika fani ya Sayansi ya Takwimu na Akili Unde (*M.Tech. in Data Science & Artificial Intelligence*) katika Taasisi ya Teknolojia ya India Madras, Kampasi ya Zanzibar.
- iii) Awe na umri usiozidi miaka 35.
- iv) Awe amefanya tahasusi za sayansi katika Kidato cha Sita na kuwa na ufaulu wa juu, hususani katika somo la Hisabati (Advanced Mathematics)
- v) Awe na GPA isiyopunguwa 3.8 katika shahada ya kwanza

F. MASHARTI YA UFADHILI

Mwanafunzi atakayepata ufadhili wa SAMIA SCHOLARSHIP EXTENDED (DS/AI+) atatakiwa kuzingatia masharti yafuatayo:

- i) Anapaswa kusoma, kuelewa na kusaini Mkataba wa Makubaliano ya Ufadhili wa Masomo kati yake na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;
- ii) Anapaswa kuwa na akaunti ya Benki kwa ajili ya fedha atakazolipwa moja kwa moja.
- iii) Mnufaika hataruhusiwa kubadilisha programu ya masomo aliyopatia ufadhili bila barua ya idhini ya maandishi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;
- iv) Mnufaika hataruhusiwa kuahirisha masomo, isipokuwa kwa sababu za kiafya, na kuthibitishwa na chuo husika;
- v) Ikiwa mnufaika ataghairi fursa ya ufadhili kabla ya kuanza masomo, atapaswa kuwasilisha taarifa ya maandishi kwenda kwa:

Katibu Mkuu
Wizara ya Elimu , Sayansi na Teknolojia
S.L.P 10,
40479, Dodoma
TANZANIA.

Barua pepe: ps@moe.go.tz

G. UTARATIBU WA KUWASILISHA MAOMBI YA UFADHILI

- i. Maombi ya Ufadhili wa Masomo yawasilishwe kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa baruapepe scholarship@moe.go.tz.
- ii. Muombaji anatakiwa aambatanishe vielelezo vyote muhimu (NIDA, Cheti cha Kuzaliwa, Vyeti vya kumalizia masomo na pamoja na Wasifu wake - CV). Aidha muombaji aweke mawasiliano yake pamoja na barua pepe na namba ya simu ,

H. MUDA WA KUWASILISHA MAOMBI

- i. Maombi ya Kuomba Ufadhili wa Masomo yawasilishwe kabla ya **April 15, 2026** chuoni **IIT Madrasa Kampasi ya Zanzibar**
- ii. Maombi ya kuomba Ufadhili wa Masomo yawasilishwe kuanzia **Juni 1** hadi **June 30, 2026**.

I. ZINGATIA

TAREHE MUHIMU ZA KUZINGATIA KWA AJILI YA MAOMBI YA IIT MADRAS, Zanzibar	
Kuanza kwa Maombi	Jumatatu 08 Disemba 2025
Mwisho wa Maombi	Jumatano, 15 Aprili 2026
Mtihani wa Mchujo	Jumapili, 26 Aprili 2026
Usaili kwa waombaji waliochaguliwa	Mwanzo wa Mei

Imetolewa na:

Katibu Mkuu

Wizara ya Elimu , Sayansi na Teknolojia

Aprill 11, 2026

Dodoma

